Teacher.co.ke

# BRAINWAVE K.C.P.E EXAMINATION PANEL

## DARASA LA NANE

## MWAKA 2022

004

BRAINWAVE PUBLISHERS

## — KISWAHILI —

Muda :Saa 1 Dakika 30

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatsi ya majibu.

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba ako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B,D na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hili.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**
**Katika kijitabu cha maswali:**

21. Nafasi iliyotengenezwa ukutani ili kuwekea vitu ni:-
    A. sefu
    B. shubaka
    C. rafu
    D. kabati

Jibu sahihi ni B (shubaka)
Katika karatasi ya majibu

20. [A] [B] [C] [D]    21. [A] [B] [C] [D]    22. [A] [B] [C] [D]    23. [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku ulivyopewa.

**Kitabu jhiki cha maswali kila kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Kutoka nambari 1 -15. Chagua jibu sahihi kujaza vihasho.**

Funzo ___1___somo la Kiswahili huhitaji ___2___ . Kiswahili ni mojawapo wa elimu ___3___ stadi muhimu sana ___4___ mawasiliano. Kujifunza kwake huanza kwa sauti. Sauti nazo huenda ___5___ . Mathalan, neno 'Mwangaza' lina silabi ___6___ . Pia anayejifunza , ___7___ kusoma sana ili ajue maneno kama vile kefle! Lo! Hamadi! Na hewala ambayo ni ___8___ . Aidha atajua mbinu ya ___9___ ambayo hupatia vitu uhai.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. la | C. za | D. cha |
| 2. | A. kuLA mumbi | B. kula muku | C. kujitoa mhanga | D. kula ari |
| 3. | A. zenye | B. yenye | C. chenye | D. lenye |
| 4. | A. kwa | B. kwenye | C. katikati | D. katika |
| 5. | A. irabu | B. silabi | C. konsonati | D. alfabeti |
| 6. | A. 5 | B. 6 | C. 3 | D. 4 |
| 7. | A. hana budi | B. hana hiari | C. hana afueni | D. hana ari |
| 8. | A. vihusishi | B. viingizi | C. viwakilishi | D. viigizi |
| 9. | A. istiara | B. tashbihi | C. chuku | D. tashihisi |

Matokeo ___10___ mtihani wa darasa la nane wa ___11___ husubiriwa kwa ___12___ . Rukia alipoyapata alipatwa na ___13___ . Hakuwa amefanya vizuri. Mwalimu wake alimshauri kujiunga na shule ya ___14___ ili kujifunza kosi ya ushonaji ushonaji. Ama kweli ___15___ .

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. za | B. ya | C. cha | D. la |
| 11. | A. kimkoa | B. kimataifa | C. taifa | D. kitaifa |
| 12. | A. ari | B. karaha | C. shauku | D. chuku |
| 13. | A. mshangao | B. raha | C. hamu | D. jazba |
| 14. | A. msingi | B. kiufundi | C. upili | D. chekechekea |

15. A. elimu ni taa gizani huzagaa
    B. ukiujua huu na huu huujui
    C. elimu ni ngao
    D. likikosa la mama na mbwa huamwa.

**Kutoka swali la 16- 30, chagua jibu sahihi.**

16. *Kanusha:*

Aliadhibiwa kwa makosa yote aliyoyafanya.

A. Aliadhibiwa kwa makosa yote asiyoyafanya

B. Hakuadhibiwa kwa makosa yote asiyoyafanya

C. Hakuadhibiwa kwa makosa yote aliyoyafanya.

D. Aliadhibiwa kwa makosa yote aliyoyafanya.

17. Nomino rungu, rafu na bahasha ziko katika ngeli gani?

A. I-ZI

B. U-Zi

C. I- I

D. U- U

18. Tambua viambishi katika kitenzi 'fungiana'

A. ian- a

B. i -an- a

C. i -a- na

D. an- a

19. Tambua sentensi yenye 'karibu' ya kuonyesha masafa.

A. Alipewa kartibu shilingi laki moja

B. Alikuwa karibu kuanguka mtoni

C. Tunaishi karibu na shule yetu

D. Ana umri wa karibu miaka sita.

20. Nyambua kitenzi <u>ogopa</u> katika kauli ya kutendesha.

A. ogofesha

B. ogovya

C. ogofyesha

D. ogofya

21. Shaibu ni kwa buda kama vile ajuza ni kwa ____________.

A. abu

B. bikizee

C. mzee

D. mkongwe

22. Chagua jibu lenye nomino iliyoundwa kutokana na kitenzi

A. Tii - mtiifu

B. Safisha- safi

C. Pungua- pungufu

D. Unda- muundo

23. Ipi si maana ya neno konga.

A. kunywa kiowevu baridi kwa mrija

B. kusanya vitu au watu pamoja

C. kuzeeka

D. kufurahisha

Teacher.co.ke

24. $^{3}/_{8}$ kwa maneno ni

A. Thumni nane

B. Thuluthi nane

C. Thumni tatu

D. Thuluthi tatu

25. *Chagua maelezo yaliyo sahihi*

A. Tarbia ni shairi lisilofuata kanuni

B. Ngonjera ni shairi la majibizano

C. Mshororo wa pili katika ubeti huitwa mleo.

D. Anayetunga na kuimba mashairi ni manju.

26. Chagua sentensi yenye ki ya kivumishi.

A. Yusuf anasomea shule ya Kihindi.

B. Mwalimu wetu hutembea kijeshi.

C. Kitoto cha maria kinalia.

D. Kioo kimeanguka kiambazani.

27. *Chagua sentensi yenye 'm' ya nafsi*

A. Mmea mpya umezinduliwa leo.

B. Mahali mlimosafishwa mmeingia watu.

C. Mwalimu alimnunulia zawadi.

D. Mtoto mzuri na mchoyo hayupo.

28. *Chagua sentensi sahihi kisarufi.*

A. Minyoo ya tumboni ina athari nyingi.

B. Nyumba ingine imejengwa leo.

C. Kule ndiko alimoingia simba.

D. Mama ana huruma nyingi kwa mayatima.

29. *Chagua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo*

Mkuki wa baba umepotea, wangu ndio huu.

A. wangu

B. wa

C. ndio

D. huu

30. Kakangu ni joka la mdimu.

A. Tashihihi

B. Istiara

C. Tashhisi

D. Kinaya

**Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha ujibu maswali 31-40.**

1. Pesa ungekuwa hewa, kwa bilashi ngepumua,
Hewa safi ni ya sawa, hukufanya kutulia,
Hewa safi hutalewa, ugomvi kapokea,
Pesa ewe kaka pesa, ni lini takuwa hewa?

2. Pesa kweli kila kitu, unachotaka kupata,
Tamaa wanayo watu, ndiposa tunavyo vita,
Megeuka kuwa chatu, pesa ndiyo damu kufuta,
Pesa ewe kaka pesa, ni lini takuwa hewa?

3. Hapa nilipo chuoni, pesa nami mejitenga,
Taka kunacha njiani, na mle mwana wa songa,
Wanifanya maskini, ndoto yangu kuboronga,
Pesa ewe kaka pesa, ni lini takuwa hewa?

4. Nasoma kupata pesa, kumaliza taka pesa,
Kupata ajira sasa, na kuishi kwema ni pesa,
Pesa nakuuliza pesa, mbona upo kunitesa?
Pesa ewe kaka pesa, ni lini takuwa hewa?

5. Wazazi nao msiba, shuleni nataka karo,
Wasumbua wangu baba, kukupata sasa kero,
Shida sa wanazibeba, pesa mekuwa mtoro,
Pesa ewe kaka pesa, ni lini takuwa hewa?

Teacher.co.ke

31. Shairi hili ni la bahari gani?
   A. Tarbia
   B. Tathlitha
   C. Uwili
   D. Ngonjera

32. Mshororo wa mwisho wa shairi hili huitwa
   A. kituo
   B. kipokeo
   C. mloto
   D. ukwapi

33. Ni sentensi ipi sawa kulingana na ubeti wa pili?
   A. Pesa imefananishwa na hewa safi.
   B. Msomaji anasoma ilikupata pesa .
   C. Tamaa ya pesa ni hatari.
   D. Pesa imeleta umaskini

34. Mwandishi wa shairi hili anatoka katika familia ya aina gani?
   A. Wahalifu
   B. Bwanyenye
   C. Wakwasi
   D. Wachochole

35. Kipande cha kwanza katika beti za shairi hili ni
   A. ukwapi
   B. utao
   C. mloto
   D. mwanzo

36. Mshororo wa pili ubeti wa tatu una mizani mingapi?
   A. Kumi na mbili.
   B. Kumi na sita.
   C. Haijalikani.
   D. Kumi na tano.

37. Kichwa cha shairi hili ni
   A. pesa
   B. katiza
   C. fanikisha
   D. ongeza

38. Neno boronga limepigwa mstari maana yake ni
   A. atili
   B. katiza
   C. fanikisha
   D. ongeza

39. Mtunzi wa shairi hili ni
   A. mfanyabiashara
   B. mkufunzi
   C. mwanafunzi
   D. kasisi

40. Anayeimba shairi huitwa_____________.
   A. malenga
   B. manju
   C. mkariri
   D. mghani

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41- 50.**

Duka la Aliki lina umaarufu katika soko la kwetu. Hili lilikuwa duka la pekee kwenye soko hilo lililouza bidhaa zilizotengenezwa kwa mikono. Mtu akifika sokoni aliweza kutambua mara moja kuwa lilikuwa wazi kutokana na baiskeli ya mwenyewe iliyoegemezwa kwenye ukuta wa duka. Mwenye duka hilo alikuwa mtu wa kwanza kunywa maji maenge. A<u>likuwa mchapa kazi aliyesifiwa hadi ya sifa katika soko zima. Na hakuna mtu ambaye hakujua jina la mwenye duka hilo Jumakosi.</u> Lakini mwenyewe alijibatiza "Alikiona" na kweli Jumakosi alikiona.

Jumakosi alikuwa mwenyeji wa kwanza wa kwetu kuhamia jijini baada ya masomo yake kugonga mwamba. Wazazi wake walifanya kila juhudi kumshawishi asiyaache masomo, lakini akatia pamba masikioni. Wazazi waliposhindwa wakasema " asiyesikia la mkuu huvunjika guu." lakini Jumakosi hakujali. Yeye alikuwa na hamu kubwa ya kukimbilia jijini alikodhani kumejaa maisha ya raha na starehe.

Hata hivyo maisha ya jijini hayakuondokea kuwa ya <u>burudani</u> kama alivyodhani Jumakosi. Yeye na vijana wengine <u>waliishia kulala kwenye majalala ya taka</u>. Chakula kilikuwa na shida kweli. Mambo yalizidi kumwendea kombo Jumakosi na wenzake. Nguo zilibadilika kabisa na kuwa nyeusi. Mwili wake ulichakaa, nywele zilitimuka na kutisha kutokana na kuchafuka na kutooga siku nyingi. Chakula kilipokosekana waliunda vigenge vya kuvamia mahoteli na maduka na kuwanyang'anya watu mali yao.

Jumakosi alifurahia maisha hayo ya mitaani, siku moja aliteuliwa kuwa kiongozi wa kigenge kilichopanga kwenda kuvamia duka moja la kuuzia chakula. Asubuhi ya "kazi" waliondoka na kujibanza karibu na lile duka ili kumtegea mwenyewe. Muda si muda, yule mwenye duka alifika kwenye mkono wake alishika kibweta. Jumakosi na kigenge walifyatuka kuelekea alipokuwa yule bwana walimpiga kumbo na kumwibia. Mwenye duka alipiga kamsa, huku kigenge kikitoroka.

Polisi waliokuwa wameshika doria karibu hapo walifyatua risasi iliyompata Isaka mguuni na kumwangusha. Risasi ziliendelea kulia na kijana aliyeitwa Kibao naye akalamba mchanga.

Jumakosi kuona hivyo mara moja aliamua kununua gari aina mguu niponye, akatimua mbio za upepo na kupiga chenga. Alipotokeza mahali salama akajificha huku akihema hadi kulipotulizana, wenzake wote walitiwa mbaroni wakiwa na maumivu. "Hapana siwezi kuishi maisha ya aina hii! Nimeponea tundu la sindano!" Alijiambia.

Tangu siku hiyo alianza maisha yaliyojaa wasiwasi. Kwa bahati nzuri alijiunga na kikundi kilichowasaidia vijana wa mitaani kuanza maisha mapya. Huko ndiko alikojifunza maarifa ya kutengeneza bidhaa kwa mikono. Baadaye Jumakosi aliamua kurudi nyumbani. Wazazi wake walifurahi walipomwona. Walijua mwenda tenzi na omo marejeo ni ngamani.

Walimsaidia kuanzisha biashara ya kujikimu, hivi ndivyo alivyoanzisha duka akaliita "ALIKIONA" Wazazi wake na watu kijijini mwetu walifurahi sana kwa kuwa mtu mwengine kabisa hata aliwaambia vijana wengine mawaidha pale dukani kwake.

41. Ni kwa nini Jumakosi alijibatiza "ALIKONA"
A. Alijifunza mambo mengi huki mjini
B. Aliona cha mtema kuni
C. Alikuwa ametoroka shule na akakiona
D. Aliponea tundu la sindano.

42. Kwa nini watu wengi walimfahamu Jumakosi ?
A. Alikuwa mchapa kazi kwa bidii
B. Aliuza bidhaa zilizotengenezwa kwa mikono
C. Alikuwa mwenyeji wa kwanza kuhamia jijini
D. Aliwauzi watu bidhaa na kuto mashauri.

43. Maana ya neno "burudani" kama ilivyotumiwa kwenye kifungu ni
A. furahi
B. starehe
C. mustarehe
D. tia moyo

44. "Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu" methali hii inahusianaje na kisa hiki
A. Jumakosi alipuuza ushauri aliopewa na wazazi wake
B. wazazi wa Jumakosi walimsaidia kuanzisha biashara
C. Jumakosi alionelea apewe funzo na ulimwengu
D. Jumakosi alikiona.

45. Methali isiyoweza kuwiana na habari hii ni
A. mui huwa mwema
B. mwenye kumchukia mwana ni hasidi wa nafsiye
C. siku za mwizi ni arubaini
D. mwenda tenzi na omo marejeo ni ngamani.

46. Mguu niponye ni gari la aina gani?
A. Mguu ukuponye
B. Kimbilia hatari
C. Kimbia kwa ajili ya usalama
D. Kukimbia kasi kwa miguu kutoroka hatari

47. Chagua sentensi isiyo sawa kulingana na taarifa hii
A. Jumakosi alipora watu mali yao
B. Maisha yake yalijaa furaha ana starehe
C. Jumakosi alikosa mahali maalum pa kulala
D. Ukosefu wa kuoga ulifanya mwili wake Jumakosi kudhoofika

48. Nini kilimfanya Jumakosi kurudi nyumbani?
A. wenzake walipotiwa mbaroni walikuwa na maumivu
B. alichoka kuishi maisha ya taabu huko mjini
C. aliponea kupigwa risasi mjini
D. wakati kitumbua kiliingia mchanga

49. "Shika doria" ni fani gani ya lugha?
A. methali
B. nahau
C takriri
D. fumbo

50. Furaha ya Jumakosi kule mjini ilitokana na
A. ufanisi wao katika uhalifu waliokuwa wakiufanya
B. alikuwa kiongozi wa vigenge vilivyonyanganya watu vitu vyao
C. huko jijini aliwez akujitawala
D. alikuwa ameyaziea matatizo